

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA SABA**

**12 APRILI, 2021**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

**KIKAO CHA SABA – TAREHE 12 APRILI, 2021**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI MKUU:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**49. MHESHIMIWA JACQUELINE NGONYANI  
MSONGOZI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Vituo vya Afya katika Kata za Tinginya, Muhimba, Kalulu, Mindu, Nalasi Magharibi na Nalasi Mashariki Wilayani Tunduru.

**50. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Hospitali ya Wilaya ya Urambo ilijengwa Mwaka 1975:-

- (a) Je, Serikali ipo tayari kuifanyia ukarabati wa majengo na miundombinu yote;
- (b) Je, ni lini Serikali itabadilisha mashine ya X-ray ya Hospitali hiyo ambayo imepitwa na wakati.



**51. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Barabara za kutoka Kata ya Kalenga kuelekea Kata za Ulanda, Maboga, Wasa, Kahanga hadi Kijiji cha Mwambao ni mbovu sana: -

Je, ni lini Serikali itahakikisha barabara hizo zinapitika hata kwa kiwango cha changarawe.

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

**52. MHESHIMIWA MICHAEL MWITA KEMBAKI (TARIME MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, ni lini Serikali itaupatia ufumbuzi mgogoro wa ardhi kati ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na wakazi wa Mtaa wa Kinyambi na Bugosi katika Halmashauri ya Mji Tarime.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**53. MHESHIMIWA DKT. STEPHEN LEMOMO KIRUSWA (LONGIDO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Uziwi ni moja ya ulemavu ambao lugha yake ni ya ishara:-

- (a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kufundisha lugha ya ishara kama moja ya somo la lazima mashuleni kwa Wanafunzi wote kuanzia elimu ya awali ili kuondoa kikwazo cha mawasiliano kati ya wenye uziwi na wanaosikia;
- (b) Je, Tanzania tuna vitabu vya kufundishia lugha ya ishara katika lugha zipi.

**54. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA  
(MBEYA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu,  
Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundombinu ya Chuo Kikuu cha Afya Mbeya pamoja na Ndaki ya Afya na Sayansi Shirikishi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam – Mbeya.

**WIZARA YA NISHATI:**

**55. MHESHIMIWA EDWARD KISAU  
OLELEKAITA (KITETO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa ajira za upendeleo kwa Vijana na fursa nyingine za kibiashara kwa Wananchi wa Jimbo la Kiteto kupitia mradi mkubwa wa kimkakati wa Bomba la mafuta (Hoima – Tanga) ambalo linapita katika Wilaya ya Kiteto.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**56. MHESHIMIWA STANLAUS SHING'OMA  
MABULA (NYAMAGANA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-


Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Kinyata kwa njia nne kutoka Mwanza Jiji kuelekea Usagara.

**WIZARA YA KILIMO:**


**57. MHESHIMIWA TWAHA ALLY MPEMBENWE (KIBITI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itahakikisha minada ya Zao la Korosho na Ufuta inafanyika kwa wakati mmoja ili kuondoa mporomoko wa bei kwa baadhi ya maeneo yanayolingana kwa misimu sawa ya kuvuna Mazao hayo.



**WIZARAYA MAJI:**



**58. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutumia maji ya Mto Ruvuma kwa ajili ya kujenga miradi mikubwa ya maji ambayo itatatua changamoto za maji katika Jimbo la Nanyamba na maeneo jirani.

**59. MHESHIMIWA DEO KASENYENDA SANGA (MAKAMBAKO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini mradi wa kusambaza maji Mji wa Makambako utaanza.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge sasa lijadili na kuidhinisha Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa kwa Kipindi cha Miaka Mitano kuanzia Mwaka 2021/22 – 2025/26.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
12 APRILI, 2021**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**